

OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI

SHULE YA SEKONDARI IBULYU

S.L.P 51

BARIADI

Barua Pepe: *sheha@gmail.com*

Tarehe:.....

Na.Simu +255 757 653 149 / +255 654 656 662

Kumb.Na.IBSS/JI/Vol 1/14

Jina la Mwanafunzi:.....

S.l.p.....

.....

FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA
(JOINING INSTRUCTION)

1.0 UTANGULIZI

- Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2019.
- Shule ya sekondari Ibulyu iko umbali wa kilometa saba(7) magharibi mwa makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Bariadi katika kijiji cha Ibulyu,kata ya sakwe,Tarafa ya Ngulyat,i Wilaya ya Bariadi Vijijini,Mkoa wa Simiyu.
- Shule inafundisha masomo ya Civics,English ,History,Geography,Kiswahili,Basic Mathematics,Chemistry,Biology na Physics.
- Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili.
- Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.BAADA YA TAREHE HIYO KUPITA NA IKIWA HUKURIPOTI SHULENI HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI.
- Ikumbukwe siku ya tarehe **11/01/2021** ndiyo siku ya kwanza ya muhula na masomo yataanza rasmi siku hiyo.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

Unatakiwa kushona sare ya shule yaani nguo maridadi,nadhifu yenye kuonesha haiba nzuri kama ifuatavyo:

2.1.1 WAVULANA

- Suruali mbili (Bluu Bahari 1 na Kijani Shule Namba moja, moja-original) yenye **U-TURN** na shati mbili (2) nyeupe mikono mifupi.
- Aina na Rangi kwa sare ya Bluu Bahari haijabadilika ni kama ile wanayoendelea kuvaa walioko shuleni, ila kwa sare ya pili imebadilika na utatakiwa kushona kitambaa kilichoambatanishwa katika fomu hii na si vinginevyo. **ENDAPO UTASHONA TOFAUTI NA KITAMBAA KILICHOAMBATANISHWA UTALAZIMIKA KUSHONA SURUALI MPYA INAYOFANANA NA KITAMBAA KILICHOAMBATANISHWA.**
- Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu.
- Mkanda wa suruali mweusi –belt ndogo.
- Soksi jozi mbili rangi nyeupe
- Tai mbili (2), Bluu Bahari 1 na Kijani Shule Namba 1 Moja
- Sweta moja ya Rangi Ya Kijani Shule yenye shingo ya v.
- Sare ya michezo kwa shule hii ni Bukta ya Rangi ya Kijani na T-shirt moja (1) ya rangi ya Njano.
- Daftari za kutosha kwa masomo yote, kalamu na mkebe wa hesabu.
- Chakula cha mwanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.1.2 WASICHANA

- Sketi mbili ndefu (Bluu Bahari 1 na Kijani Shule Namba moja, moja-Original 1). Mashono sketi ya Rinda Boksi (Rinda moja mbele katikati, Na Rinda la pili nyuma katikati), urefu wa sketi unaofika katika kifundo cha mguu. **ENDAPO UTASHONA TOFAUTI NA MAELEKEZO UTALAZIMIKA KUSHONA SARE MPYA INAYOENDANA NA MAELEKEZO YA SHULE.**
- Aina na Rangi kwa sare ya Bluu Bahari na Kijani Shule Namba moja haijabadilika ni kama ile wanayoendelea kuvaa walioko shuleni. **ENDAPO UTASHONA TOFAUTI NA SARE INAYOTAKIWA UTALAZIMIKA KUSHONA SARE MPYA INAYOKUBALIKA.**
 - Rangi ya hijabu ifanane na Sare za shule.
 - Shati mbili (2) za Rangi nyeupe mikono mifupi.
 - Soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe zisizo na mapambo ya aina yoyote.
 - Viatu vya ngozi visivyo na kisigino kirefu.
 - Tai mbili (2), Bluu Bahari 1 Na Kijani Shule Namba moja, Moja-Original.
 - Sare za michezo Sketi Za Rangi ya Kijani na T-shirt moja (1) kwa wasichana ya rangi ya Njano.
 - Daftari za kutosha kwa masomo yote, kalamu na mkebe wa hesabu.
 - Chakula cha mwanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.